KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 1

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM

Toleo la Februari, 2010

**Zimetolewa na:**
**Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM**

**Bei Sh.500/=**

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 2

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 3

# KANUNI
# ZA
# UCHAGUZI WA CCM

**Toleo la Februari, 2010**

**“Tangu tuingie katika mfumo wa vyama vingi Julai 1, 1992, Viongozi wetu wa kuchaguliwa katika Chama wamekuwa wakifanya kazi za CCM kwa kujitolea ..... Kufanya kazi za Chama kwa kujitolea ndiyo mila inayoendana na mifumo ya vyama vingi duniani kote ..... CCM itahakikisha kuwa msimamo huu wa kujitolea unaimarika, kukubalika na kuenezwa ndani ya Chama.”**

**(ILANI ya Uchaguzi ya CCM,
Oktoba, 1995)**

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 5

## YALIYOMO

1. Utangulizi ..... 1
Uongozi ..... 2

**2. FUNGU LA KWANZA**
i. Fomu za kuomba nafasi ya Uongozi ..... 5
ii. Vikao vya kuwachuja waombaji wa nafasi za Uongozi ..... 6
iii. Vikao vya Uchaguzi ..... 10
iv. Utaratibu wa kupiga kura ..... 13
v. Utaratibu wa kuhesabu kura na kutangaza matokeo ..... 14
vi. Nafasi za Uongozi ambazo ni kazi za muda wote na Uwakilishi ..... 16
vii. Malalamiko ya Uchaguzi ..... 18
viii. Miiko ya kuzingatiwa wakati wa shughuli za uteuzi na uchaguzi ..... 24

**3. FUNGU LA PILI**
i. Uchaguzi wa Viongozi wa ngazi ya Shina ..... 28
ii. Utaratibu wa kuomba nafasi za Uongozi .. 29

**4. FUNGU LA TATU**
i. Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Tawi na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi... 33
ii. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri kuu ya Tawi ..... 37

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 6

**5. FUNGU LA NNE**

i. Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Kata/Wadi na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi... 39
ii. Utaratibu wa Uchaguzi ..... 40
iii. Uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi ... 42

**6. FUNGU LA TANO**

i. Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Jimbo na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi .....
45
ii. Utaratibu wa Uchaguzi ..... 46
iii. Uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Jimbo.....48

**7. FUNGU LA SITA**

i. Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Wilaya na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi .....50
ii. Utaratibu wa Uchaguzi ..... 53
iii. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya .....55

**8. FUNGU LA SABA**

i Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Mkoa na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi.... 57
ii. Utaratibu wa kuchuja majina ya Waombaji
58
iii. Utaratibu wa Uchaguzi .....60
iv. Uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa .....62

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 7

**9. FUNGU LA NANE**

i. Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Taifa na Utaratibu wa kuomba nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa..... 64

ii. Utaratibu wa kuwachuja waombaji wa nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ....64

iii. Utaratibu wa kupendekeza wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa MWenyekiti wa CCM.....65

iv. Utaratibu wa Uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa pamoja na Mwenyekiti wa CCM na Makamu wake wawili ..... 66

v. Uchaguzi wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ..... 67

vi. Uchaguzi wa Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Mkuu wa Chama na Wakuu wa Idara makao Makuu ya Chama ..... 70

vii. Uteuzi wa Makatibu wa MIkoa..... 71

**10. FUNGU LA TISA**

i. Uchaguzi wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi ..... 72

ii. Kugawanywa kwa Kijiji, Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya na Mkoa ..... 74

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 8

# UTANGULIZI

(i) Katika kuimarisha kazi yake ya kuongoza Mapinduzi yetu ya Kijamaa, Chama Cha Mapinduzi hakina budi kuhakikisha kuwa viongozi wake wote, wa kuchaguliwa au kuteuliwa, ni waumini wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na kwamba ni Wanamapinduzi wa kweli kweli wasioyumba wala kubabaika.

(ii) Kwa mujibu wa Katiba ya CCM, Uchaguzi Mkuu wa Chama hufanyika kila baada ya kipindi cha miaka mitano. Kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kutokana na chaguzi za nyuma tangu CCM izaliwe mwaka 1977 na pia tangu mageuzi ya mfumo wa vyama vingi vya Siasa yafanyike mwaka 1992, CCM inalazimika wakati wa chaguzi zake zote kuwa makini zaidi katika kuhakikisha kwamba inachagua viongozi wenye uwezo wa kuhimili vishindo vya ushindani wa kisiasa katika ngazi zote za uongozi.

(iii) Ili tuweze kupata ufanisi mkubwa zaidi katika chaguzi zetu sharti tufanye juhudi ya kuepuka kasoro zote zinazogusa maadili ya Chama na zile za utendaji ambazo zinawezesha watu wasiostahili kuchaguliwa waweze kupenya kwenye uongozi ama kwa rushwa au kwa hila. Kwa sababu hiyo lazima Maadili ya Chama yazingatiwe kwa ukamilifu na vikao vyote vinavyochuja na kuteua wagombea.

(iv) Aidha, pamoja na kuwapo kwa kanuni hizi, Katibu Mkuu wa CCM aweza kutoa miongozo ya ziada kuhusu masuala yanayopaswa kuzingatiwa katika chaguzi za Chama Cha Mapinduzi.

(v) Wajibu wa Chama wakati wote ni kujenga na kudumisha uongozi bora nchini. Uongozi bora ni moja ya masharti ya maendeleo yaliyomo katika Azimio la Arusha. Kwa hiyo Chama kinalazimika kuujenga na kuudumisha, hasa ndani ya Chama chenyewe.

## UONGOZI

1. Uongozi bora katika Chama chetu, una masharti matano yafuatayo:-
   (1) Kiongozi wa Chama akinai maadili ya Chama, na asiwe mtu wa kuyumba katika masuala ya msingi ya Ujamaa wetu.
   (2) Awe na uwezo wa kazi anayotarajiwa kufanya katika ngazi yake ya uongozi kulingana na wakati uliopo.
   (3) Awe na uwezo wa kuhimili na kuvishinda vishindo/vitimbi vya wapinzani.
   (4) Kwa kiongozi wa kuchaguliwa, lazima wanachama wamchague kiongozi wao kwa hiari na uhuru kabisa, na kwa njia ya haki. Vinginevyo tutajenga Chama cha wachache tu ambacho wanachama wengi hawana kauli nacho.
   (5) Muda wa Uanachama wa kila mgombea usipungue miaka mitano mfululizo ili Chama kiwe na uhakika na msimamo wake. Hii inawahusu hata wanaorudi CCM baada ya kujiuzulu, kuachishwa au kufukuzwa uanachama. Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu

ya Taifa ina uwezo wa kuamua kwa kadri itakavyoona inafaa juu ya utekelezaji bora wa sharti hili la Kanuni kwa manufaa ya Chama. Kamati Kuu imekasimu madaraka yake kwa Kamati za Siasa za Wilaya kuhusu chaguzi za ngazi ya Shina hadi Tawi; na kwa Kamati za siasa za Mikoa kuhusu chaguzi za ngazi za Kata/Wadi na Jimbo.

**(vi) Katika kitabu cha TANU na Raia twasoma hivi:**

"Kila mmoja wetu aliye katika hali ya uongozi, toka President mpaka Chairman wa Kijiji; toka Secretary General mpaka Secretary wa Tawi, hana budi ajiulize: Ikiwa nilichaguliwa kwa kura, hizo kura nilizipataje? Nilizipata kwa hila, kwa rushwa, kwa vitisho au kwa ujanja wa aina yoyote, au nilizipata kwa hiari ya wapiga kura wenyewe?

Asili ya uongozi wetu ni mbili:- Ya kwanza ni WATU. Uongozi wetu hauna budi utokane na watu wa nchi hii, bila hila, bila rushwa, au bila vitisho na bila ujanja wa aina yoyote. Tunapofika katika hali ya uongozi kwa kupitia mlango wa hila, au rushwa, au vitisho au ujanja wa aina nyingine yoyote basi hatukutokana na watu wenyewe.

Ya pili ni HAKI. Lakini haki ni haki ya watu, siyo kwa majani au kwa miti. Tunapofika katika uongozi kwa njia yoyote ambayo si ya haki, ni wazi kwamba haiwezekani tuwe tumetokana na watu wenyewe.

Watu na Haki ni misingi ya uongozi ambayo haiachani....."

**(TANU na Raia, 1962)**

(vii) Uongozi bora unaendelea kusisitizwa na kuzingatiwa na maandishi yafuatayo:-

(1) "Ko kote aliko, mawazo na juhudi ya Kiongozi, fikra na kazi yake wakati wote lazima ziwe mfano mwema na bora wa utekelezaji wa wajibu wake kwa viongozi wenziwe na kwa watu wengine.

(2) Msingi wa wajibu wa kiongozi lazima daima utokane na imani ya kutumikia wananchi kwa dhati katika kuwasaidia na kuwaendeleza wainue hali zao za maisha na kuzifanya zilingane.

(3) Ni mwiko kwa Kiongozi kutumia wadhifa wake kwa ajili ya hamu yake, kwa upendeleo au kwa chuki na ni mwiko kutumia vyombo vya Chama au Serikali yake kwa kazi yoyote ya binafsi au kwa shughuli yoyote ya binafsi au kwa shuhguli yoyote isiyohusiana na wajibu wake akiwa kiongozi."

**(Katiba ya ASP)**

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 13

# FUNGU LA KWANZA

## KANUNI ZA JUMLA

### Fomu za Kuomba Nafasi ya Uongozi

1. Ukiondoa waombaji wa nafasi za Mwenyekiti na Makamu wawili wa Mwenyekiti ambao kwa mujibu wa Katiba ya CCM watapatikana kwa njia ya kupendekezwa na Kamati Kuu na kuteuliwa na Halmashauri kuu ya Taifa, kila mwanachama anayeomba nafasi yoyote ya uongozi wa Chama atatakiwa kwanza kujaza Fomu ya kuomba nafasi ya uongozi. Mwombaji aweza kuipata fomu hiyo katika Ofisi yoyote ya Chama, lakini baada ya kujaza fomu yake itabidi aiwasilishe kwa Katibu wa Chama wa ngazi ya uongozi anaouomba, au kama itakavyoelekezwa katika Kanuni hizi na kufuata Ratiba iliyowekwa ya utekelezaji wa shughuli za uchaguzi unaohusika. Haitakuwa lazima kwa mwombaji yeyote kuwasilisha Fomu yake yeye mwenyewe binafsi. Anaweza kuiwasilisha kwa kuituma kwa Posta, au kwa njia nyingine inayofaa mradi tu ajihakikishie kuwa itafika panapohusika katika muda uliowekwa.

   Kila mgombea anayechukua fomu ya kuomba uongozi katika Chama, atachangia kiasi cha fedha kwa kiwango kitakachokuwa kimewekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uchaguzi unaohusika kwa madhumuni ya kuimarisha Chama.

2. Kutakuwa na Fomu za uongozi za aina mbili zifuatazo:-

   (i) Fomu ya kuomba Uongozi wa Chama ngazi ya Shina hadi Kata/Wadi na Jimbo.

   (ii) Fomu ya kuomba Uongozi wa Chama ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa.

   Kamati Kuu itaandaa Fomu zinazotakiwa kwa kila Uchaguzi Mkuu wa CCM utakaofanyika.

**Vikao vya Kuwachuja Waombaji wa Nafasi za Uongozi**

3. Waombaji wa nafasi zote za Uongozi watachujwa na Vikao vinavyohusika. Fomu haitakuwa njia pekee ya kupata Taarifa sahihi ya mgombea. Wajumbe, hasa wa vikao vya uchujaji, watajadiliana kuhusu Uanachama wake, yaani kama anatimiza masharti yote ya Uanachama (ibara ya 8 ya Katiba ya Chama) na kama anatekeleza kwa ukamilifu wajibu wa Uanachama (ibara ya 15 ya Katiba ya Chama), kifungu cha 51 cha Kanuni za Utendaji Kazi za Uongozi katika Chama na Miiko ya Uongozi iliyomo katika Katiba ya Chama ibara ya 18.

   Baada ya kujiridhisha na ukamilifu wa Uanachama, kikao kitapima mambo muhimu kama ni muumini wa kweli wa Ujamaa na Kujitegemea. Aidha maisha yake ya kila siku yatazingatiwa. Pili kitapima uwezo wake wa kumudu nafasi ya Uongozi anayoiomba, na kama ana uzoefu wowote wa Uongozi.

4. Mikutano ya Vikao vya kuwafikiria na kuwachuja waombaji wa nafasi za uongozi itafanyika kwa kufuata Ratiba iliyotolewa kwa ajili hiyo.

5. Baada ya mwombaji kujadiliwa, maoni na mapendekezo ya kikao juu ya mwombaji yaandikwe kwenye Kumbukumbu za Kikao na kwenye fomu yake aliyojaza na atapewa alama inayolingana na maelezo hayo ambayo yanazingatia sifa alizonazo mwombaji. Alama zitakazotumika ni A, B, C, D na E kwa kuzingatia mpangilio ufuatao:-

   (1) **"A"** itatolewa kwa mwombaji anayetimiza Miiko, Masharti na sifa zote za uongozi kama ilivyo katika kifungu (viii) cha Kanuni hizi na katika vifungu vya 17 na 18 vya Katiba ya Chama; na anayetimiza sifa za nyongeza zifuatazo:-

   (i) Awe ni muumini na mtekelezaji kwa vitendo wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea asiyetiliwa mashaka; na kwamba Itikadi, Msimamo na Tabia yake vithibitishe kuwa ni vya kijamaa.

   (ii) Awe anaheshimu Miiko ya Kiongozi ambayo imetamkwa na Katiba ya CCM.

   (iii) Awe na Uadilifu na Uaminifu kwa Chama chake katika tabia na mwenendo wake, anayeheshimu maadili ya CCM na ambaye kwa maneno na vitendo vyake hawafanyi wananchi wapoteze imani yao kwa CCM.

(iv) Awe tayari kushirikiana na Viongozi wenzake katika kuunga mkono jitihada zote za kudumisha Maadili mema nchini.

(v) Awe na uwezo mkubwa wa kuwahamasisha na kuwashirikisha wana-CCM na wananchi katika kazi za kujenga Taifa na kutafuta mbinu za kuondoa kero zao kwa kuunganisha nguvu zao.

(vi) Awe na uwezo mkubwa wa kuongoza kwa nafasi anayoiomba kutokana na uzoefu aliouonyesha huko nyuma, hasa katika Taasisi mbalimbali za Umma au Jumuiya ya Wananchi; na ionekane wazi kwamba atamudu nafasi anayoiomba.

(vii) Awe ameonyesha kwa vitendo na kwa nadharia uwezo wa kueleza Siasa ya Chama, kuitetea kuweka malengo, kuandaa watu, kusimamia utekelezaji wake na kupima matokeo ya utekelezaji huo.

(viii) Awe tayari wakati wowote kujikosoa, kukosolewa na kukosoana kama mbinu ya kujiimarisha ndani ya Chama katika ngazi ya uongozi anaouomba.

(2) **"B"**Itatolewa kwa mwombaji anayetimiza sifa, miiko na masharti yote ya uongozi na ana msimamo lakini anapungukiwa moja ya sifa za nyongeza (v) hadi (vii) hapo juu.

(3) **"C"** itatolewa kwa mwombaji anayetimiza sifa, miiko na masharti yote ya uongozi, lakini msimamo wake haujajitokeza au uwezo wake ni wa wastani tu, ambaye anaweza kupewa nafasi ya kujaribiwa.

(4) **"D"** itatolewa kwa mwombaji ambaye hana dosari lakini hana msimamo unaofaa, wala uwezo wa kumudu uongozi wa aina anayoiomba.

(5) **"E"** itatolewa kwa mwombaji ambaye amekataliwa kwa sababu ana dosari. Dosari zake zitajwe waziwazi katika muhtasari wa kikao cha uteuzi wa mwisho.

6. Licha ya kuandika maoni ya jumla kwenye muhtasari wa kikao, maoni/mapendekezo ya vikao vinavyowajadili waombaji wa nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama yataandikwa pia kwenye Fomu walizojaza waombaji hao katika sehemu zinazohusika. Katibu wa kila kikao ahakikishe kwamba ameyaandika maoni/mapendekezo ya mkutano wake kwa ukamilifu ili kuvisaidia vikao vya uteuzi wa mwisho.

7. Ili kuziba mwanya wa mtu yeyote mwingine kuweza kughushi maelezo au alama ya mwombaji yeyote nje ya kikao, maelezo na alama zitakazotolewa kwa kila mwombaji zitathibitishwa na kikao kinachohusika kabla

ya kufunga mkutano wake. Hazitasubiri kuthibitishwa katika mkutano unaofuata kama ilivyo katika mikutano ya kawaida.

8. Endapo yupo mwombaji ambaye ni mjumbe wa kikao hicho, atalazimika kuondoka kwenye kikao wakati zamu yake ya kujadiliwa itakapofika, lakini ataendelea na kikao mara zamu yake ya kujadiliwa itakapomalizika. Atafanya hivyo hivyo wakati wa kuthibitishwa maelezo na alama aliyopewa kwa mujibu wa ibara ya 7 hapo juu.

9. Kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho wa waomba uongozi kitateua idadi ya wagombea kwa kuzingatia ibara ya 33 (vifungu vya 9, 10, na 11) ya Kanuni hizi. Hairuhusiwi mwombaji wa nafasi yoyote ya uongozi kuondoa jina lake baada ya kuteuliwa kugombea bila idhini ya kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho.

## VIKAO VYA UCHAGUZI

10. Mikutano ya Uchaguzi itafanyika kufuata ratiba itakayotolewa kwa ajili ya uchaguzi unaohusika. Ni marufuku kampeni ya aina yoyote kufanyika siku yenyewe ya uchaguzi. Shughuli zote za kampeni zitamalizika siku ambayo inatangulia siku ya uchaguzi wenyewe, ili uchaguzi uweze kufanyika katika mazingira ya utulivu na amani.

11. (a) Kila Mkutano wa Uchaguzi utasimamiwa na viongozi wasiozidi watatu, walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa madhumuni hayo. Kamati za Siasa za kila ngazi zitateua wasimamizi watakaosimamia uchaguzi wa ngazi ya chini yake. Kamati Kuu itateua viongozi wa kusimamia uchaguzi wa ngazi za mkoa na ngazi ya Taifa.

Aidha unapofika wakati wa uchaguzi wa kuchagua Mwenyekiti wa muda katika mikutano ya uchaguzi mjumbe ambaye ni mgombea wa nafasi yoyote katika mkutano husika hatakuwa na haki ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo.

(b) Kazi ya wasimamizi hao itakuwa ni kuhakikisha kuwa haki inatendeka na kwamba maagizo ya Katiba ya Chama pamoja na Kanuni hizi yanafuatwa kwa ukamilifu. Wasimamizi wa uchaguzi pia watakuwa na uwezo wa kutoa uamuzi wa pamoja juu ya jambo lolote linalohusu utaratibu litakalotokea wakati wa mkutano wa uchaguzi endapo jambo hilo litafafanuliwa katika kanuni hizi.

12. Waombaji wote walioteuliwa kugombea watapewa nafasi ya kujieleza mbele ya Mkutano wa Uchaguzi unaohusika.

13 Katika uchaguzi ambapo wanaohitajika kuchaguliwa ni zaidi ya mmoja, kama vile Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa kutoka Wilayani, au Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka Zanzibar n.k. kila mpiga kura atapiga kura katika karatasi moja kwa idadi maalum inayotakiwa. Mpiga kura atakayepiga kura zaidi au pungufu ya kura zinazotakiwa, kura yake itakuwa imeharibika.

Katika uchaguzi huu wa kujaza nafasi nyingi kwa pamoja, endapo idadi ya wagombea walioteuliwa kwa ajili ya uchaguzi wa nafasi hizo ni wachache kuliko nafasi zilizopo, au kama haizidi idadi ya nafasi hizo, wajumbe watapiga kura “ndiyo” na “hapana” kwa kila mgombea.

14. Mwanachama mwenye haki ya kupiga kura ni yule ambaye ni mjumbe halali kikatiba wa kikao cha uchaguzi kinachohusika.

15. Chama kitaendelea kuhimiza wanachama wake wote watekeleze ipasavyo wajibu wao wa kulipa ada za kila mwezi za Uanachama wao. Lakini kuchelewa kulipa ada haitakuwa kizuizi kwa mwanachama yeyote wa CCM kushiriki katika shughuli za kuwachagua viongozi wake.

16. Ili kuhakikisha kwamba watu wasiokuwa na haki ya kupiga kura hawapigi kura, Mikutano inayofanya Uchaguzi itahudhuriwa tu na wajumbe ambao ni wajumbe wa mkutano huo

kwa mujibu wa Katiba ya Chama, pamoja na maafisa wanaotakiwa kuhudumia mkutano huo na Wasaidizi wao. Wajumbe wa kukaribishwa hawataruhusiwa. Endapo itakuwa lazima mikutano ya uchaguzi kuwa na wakaribishwa itabidi sehemu yao ya kukaa itengwe ili wasichanganyike na wajumbe wa mikutano. Wasimamizi na wengine wote wasio wajumbe hawatapiga kura. Karatasi za kupigia kura zisigawiwe mpaka wagombea wote wamemaliza kujieleza.

**Utaratibu wa Kupiga kura:**

17. Uchaguzi wowote wa Chama utafanyika kwa kura ya siri kuanzia ngazi ya Shina hadi ngazi ya Taifa kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa mapema kwa ajili hiyo na uongozi wa ngazi inayohusika. Kiwango cha mahudhurio ya Wajumbe katika Mikutano yote ya CCM ya uchaguzi (Akidi ya Wajumbe) ni zaidi ya nusu ya Wajumbe walio na haki ya kuhudhuria katika kikao kinachohusika kwa mujibu wa Katiba ya CCM.

18. Katika uchaguzi wa Chama wa ngazi zote, utaratibu wa kupiga kura utakuwa kama ifuatavyo:-
    (i) Unapofika wakati wa kupiga kura, kila mjumbe mwenye haki ya kupiga kura katika uchaguzi huo, na kwa kufuata

mpangilio uliowekwa, ataondoka mahali alipoketi na kwenda mahali maalum palipotengwa kwa ajili ya zoezi la upigaji kura.

(ii) Mjumbe huyo atakabidhiwa karatasi moja ya kupigia kura, atapiga kura yake kwa siri, na kisha ataitumbukiza karatasi hiyo kwenye sanduku la kura litakalokuwa limewekwa mahali pa wazi.

19. Mikutano yote ya Uchaguzi itaanza mapema iwezekanavyo kabla na siyo baada ya saa nne asubuhi. Kwa hiyo maandalizi yafanywe kwa makini ili kuhakikisha kwamba wajumbe wahusika wanakuwa tayari katika viti vyao kabla ya saa iliyopangwa. Hatua hii ni kuepukana na tabia ya kufanya vikao vya uchaguzi usiku kwa sababu tu ya kuchelewa kuanza.

**Utaratibu wa kuhesabu kura na kutangaza matokeo**

20. Kazi ya kuhesabu kura itasimamiwa na Kamati ya Watu Watatu itakayokuwa imeteuliwa mapema kwa ajili hiyo.

(a) Katika uchaguzi wa kujaza nafasi moja, ambapo wagombea hawawezi kuzidi watatu, kila mgombea anaweza kuteua mwakilishi wake mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano unaohusika, atakayehudhuria kama shahidi wake

katika zoezi la kuhesabu kura zinazomhusu. Hata hivyo, mgombea mwenyewe aweza, akipenda, kuhudhuria yeye mwenyewe katika zoezi hilo la kuhesabu kura zinazomhusu.

(b) Katika uchaguzi wa kujaza nafasi za makundi, hususani ya Wanawake, Vijana na Wazazi, ambapo wagombea kwa kawaida huwa ni wengi kiasi kwamba haiwezekani kwa kila mgombea kupewa fursa ya kuteua mwakilishi wake, itabidi wagombea wa makundi hayo wakubali kwamba Kamati iliyoteuliwa kusimamia kazi ya kuhesabu kura ndiyo itakuwa mashahidi wao katika zoezi hilo. Isipokuwa kwamba kama kundi linalohusika linawagombea wachache tu wasiozidi kumi na watano, kila mgombea anaweza kumteua mwakilishi wake

21 (a) Kazi ya kuhesabu kura itafanyika tu wakati ambapo kuna mwanga wa kutosha na wa kuaminika na mahali ambapo kuna ulinzi na usalama madhubuti.

(b) Kiwango cha kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa. Kura halali zilizopigwa ni kuondoa kura zilizoharibika. Katika uchaguzi wa kujaza nafasi nyingi kwa pamoja (Uchaguzi wa kundi) ushindi

utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura alizopata mwombaji.

(c) Katika kutangaza matokeo ya kura, mtiririko utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Idadi ya kura zilizopigwa

(ii) Idadi ya kura zilizoharibika

(iii) Idadi ya kura halali zilizopigwa

(iv) Matokeo ya kura yatangazwe kuanzia chini yaani aliyepata kura chache zaidi na kuendelea hadi anayeongoza kwa wingi wa kura.

(v) Mwisho ni kutangaza rasmi washindi .

**Nafasi za uongozi ambazo ni kazi za Muda wote na Nafasi za Uwakilishi.**

22. Mwanachama ambaye anaomba nafasi ya uongozi ambayo ni kazi ya muda wote, hataruhusiwa kushika nafasi ya aina hiyo zaidi ya moja katika Chama isipokuwa kama Kamati Kuu imeamua vinginevyo.

Kamati Kuu yaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati za Siasa za Mikoa kuhusu uteuzi wa wagombea wa ngazi ya Mtaa Kijiji na Diwani wanaoomba kushika nafasi za muda wote, zaidi ya moja ndani ya Chama.

23. Nafasi za uongozi zenye kazi ya muda wote ni kama vile Mwenyekiti wa Tawi la Kijiji au la Mitaani, Mwenyekiti wa Kata/Wadi, Mwenyekiti wa Jimbo, Mwenyekiti wa Wilaya, Mwenyekiti wa Mkoa, Makatibu wa Halmashauiri Kuu wa ngazi zinazohusika, Diwani, Mwakilishi na Mbunge. Nafasi nyingine za uongozi ni za Uwakilishi tu, hivyo wahusika wataendelea na kazi zao za kawaida isipokuwa wakati wa vikao.

24. Katibu wa Chama wa ngazi yoyote na Afisa au Mtumishi mwingine yeyote wa Chama na Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM akichaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi yenye kazi ya muda wote atakuwa katika likizo isiyokuwa na malipo kwa kipindi chote atakachoshika nafasi hiyo ya uongozi.

    Aidha, Mtendaji wa Chama au Jumuiya wa ngazi ya chini haruhusiwi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya ngazi ya juu yake au Kamati Kuu. Iwapo mhusika kabla ya kuchaguliwa/kuteuliwa kuwa Mtendaji wa Chama ni mjumbe wa Kamati ya Siasa ya ngazi ya juu au Kamati Kuu, atalazimika kujiuzulu uongozi huo mara baada ya kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa Mtendaji wa ngazi ya chini.

25. Kwa kuwa nafasi zote za uongozi ni za Chama, mwombaji anaweza kuteuliwa kuomba nafasi tofauti na ile anayopendelea endapo kufanya hivyo ni kwa maslahi ya Chama.

## Malalamiko ya Uchaguzi

26 (1) Kutakuwa na nyakati mbili za kuwasilisha na kushughulikia malalamiko ya uchaguzi katika chaguzi zote za Chama.

(a) Kabla na wakati wa vikao vyenyewe vya uchaguzi.

(b) Baada ya uchaguzi kumalizika.

(2) Malalamiko yaweza kuwasilishwa kabla, au wakati wa vikao vyenyewe vya uchaguzi, kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Mlalamikaji atawasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa CCM wa ngazi ile ambapo uchaguzi unafanyika.

(b) Ili kuepuka majungu, na kwa ajili ya kulinda haki, malalamiko yatawasilishwa kwa maandishi, ambayo pia itabidi yaainishe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa.

27 (1) Baada ya kupokea lalamiko lolote, Katibu wa CCM wa ngazi inayohusika ataitisha mara moja kikao cha Kamati ya Siasa ya ngazi hiyo ambayo ndiyo Kamati ya Udhibiti kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Kamati za Siasa, au Kamati Kuu kwa ngazi ya

Taifa, zitakuwa na mamlaka ya kushughulikia Taarifa za ukiukwaji wa Maadili au wa Kanuni au Katiba ya Chama wakati wowote, kabla na pia wakati wa uchaguzi wenyewe. Kamati hizo zinapaswa kudhibiti makosa ya uchaguzi pale pale yanapofanyika, bila kusubiri malalamiko yatolewe baada ya uchaguzi kumalizika.

(3) (a) Endapo wakati wa uchaguzi wenyewe Kamati ya Siasa itabaini kuwapo kwa vitendo vilivyokatazwa katika Kanuni hizi, na ili ratiba ya uchaguzi huo isiathirike, kikao cha Kamati hiyo kitafanyika mara moja ili kutafakari tukio linalohusika na kulitolea uamuzi.

(b) Katika uchaguzi unaofanywa na Mkutano Mkuu wa Taifa, endapo wakati wa uchaguzi Kamati Kuu itabaini kuwapo kwa vitendo vilivyokatazwa katika Kanuni hizi, Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa kitafanyika mara moja ili kutafakari tukio linalohusika na kulitolea uamuzi.

(4) Malalamiko yoyote ambayo Kamati ya Siasa itaridhika kuwa hayana ukweli yatakataliwa. Lakini kwa malalamiko ambayo yatathibitika kuwa yana ukweli, Kamati hiyo itakuwa na mamlaka kuwadhibiti wahusika kama ifuatavyo:-

(a) Pale ambapo Kamati husika itaridhika kwamba tuhuma za rushwa dhidi ya

mgombea fulani au wakala wake zimethibitika kuwa ni za kweli, basi Kamati hiyo itapeleka haraka taarifa ya tukio hilo kwa vikao vya ngazi za juu yake, ili hatua ziweze kuchukuliwa dhidi yake kwa mujiibu wa Kanuni ya 33(2).

(b) Kwa wale watuhumiwa wa vitendo ambavyo havihusiani na rushwa lakini bado vinakiuka Kanuni za Uchaguzi wa Chama, hususani zile zinazokataza matumizi ya mabango, vipeperushi, kampeni chafu, vurugu za wapambe au wapiga debe, matusi na upotoshaji wa makusudi wa sifa za wagombea wengine wanaoshindana nao, hawa watadhibitiwa na Kamati ya Siasa inayohusika kwa kuwakemea na kuwaonya mapema waache mara moja kufanya vitendo hivyo, na watuhumiwa hao watalazimika kutii amri iliyotolewa na Kamati hiyo.

(c) Katika kushughulikia malalamiko yanayotolewa baada ya uchaguzi kumalizika chini ya Kanuni ya 26 ya Kanuni hizi, endapo Kiongozi yeyote atathibitika kwamba alipata ushindi huo kutokana na rushwa, basi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa ibara ya 33(2) ya Kanuni hizi.

(d) Kwa upande wa watuhumiwa ambao ni viongozi wa CCM wa ngazi yoyote wanaothibitika kujihusisha na vitendo vya kumbeba na kumpigia debe mgombea mmojawapo miongoni mwa wagombea walioteuliwa rasmi na Chama, Kamati ya Udhibiti ya ngazi inayohusika itakuwa na mamlaka ya kumkemea na kumpa onyo au onyo kali au karipio, pamoja na kumtaka Kiongozi mhusika aache vitendo vyake hivyo mara moja, na Kiongozi aliyetakiwa kufanya hivyo atapaswa kutii amri hiyo.

(e) Endapo makosa ya aina hiyo yatafanywa na kiongozi ambaye ni Katibu wa CCM wa ngazi yoyote, ambaye kwa wadhifa wake huo anakuwa pia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi katika eneo lake, au ni Afisa, au Mtumishi mwingine wa CCM wa ngazi yoyote, Kamati ya Udhibiti ya ngazi ya juu yake ikisha kuridhika kuwa tuhuma zimethibitika kuwa ni za kweli, itapeleka Taarifa ya Maandishi mara moja kwa Katibu Mkuu wa Chama, ambaye kutokana na taarifa hiyo atamchukulia hatua za kinidhamu zinazohitajika.

28. (1) Malalamiko yaweza pia kuwasilishwa baada ya uchaguzi kumalizika kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Mara baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa, mwanachama yeyote aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uongozi inayohusika, endapo anayo malalamiko kuhusu uchaguzi huo, atawasilisha malalamiko yake hayo kwa Katibu wa Chama wa ngazi ya juu inayofuata.

Isipokuwa kwamba kama uchaguzi unaolalamikiwa ni wa ngazi ya Taifa, malalamiko yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Chama.

(b) Ili kuepuka majungu, na kwa ajili ya kulinda haki, malalamiko yatawasilishwa kwa maandishi ambayo pia itabidi yaainishe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa. Mlalamikaji lazima pia ataje majina yake kamili na anuani yake.

(2) Malalamiko hayo lazima yawasilishwe katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne tangu siku ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi unaolalamikiwa.

(3) Kikao kinachoshughulikia malalamiko baada ya uchaguzi kumalizika kwa mujibu wa fasili ya (1) ya Kanuni hizi, kitakuwa vile vile na uwezo wa kusikiliza rufaa kutoka kwa Kamati ya Siasa inayohusika, pale ambapo Kamati husika ilitoa amri zilizotajwa katika Kanuni ya 27(4) (a) na (d) lakini wahusika hawakutii amri hizo, au rufaa kutoka kwa mgombea au kiongozi anayehisi

kuwa aliathirika kutokana na maamuzi fulani ya Kamati ya Siasa iliyomdhibiti.

(4) Kila mgombea wa nafasi yoyote ya uongozi katika Chama azingatie kuwa uchaguzi wa viongozi wa CCM wa ngazi zote ni suala la kazi ya Chama ndani ya Chama. Hivyo CCM ina uwezo kamili wa kuyatafutia ufumbuzi malalamiko yote ya uchaguzi ndani ya Chama chenyewe bila ya kushawishika kuyapeleka Mahakamani.

29. Malalamiko yatakayowasilishwa kinyume cha Kanuni hizi za Uchaguzi hayatashughulikiwa.

30. Malalamiko ya Uchaguzi yatashughulikiwa bila kuchelewa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya ngazi inayohusika na kutoa uamuzi juu ya malalamiko hayo. Endapo uamuzi uliotolewa unahitaji hatua zichukuliwe ambazo kwa mujibu wa Katiba ya CCM ziko nje ya uwezo wa ngazi inayohusika, Kamati hiyo itatoa taarifa na mapendekezo yake mara moja kwa kikao cha Chama chenye uwezo wa kuchukua hatua iliyopendekezwa.

31. Malalamiko yote yanayohusu mambo ya Uchaguzi lazima yawe yameshughulikiwa na kumalizwa na vikao vyote vinavyohusika katika muda usiozidi miezi sita tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi unaolalamikiwa.

32. Kamati Kuu ndicho Kikao cha Chama chenye uamuzi

wa mwisho katika malalamiko yote yanayohusu uchaguzi wa viongozi wa CCM wa ngazi zote kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**Miiko ya kuzingatiwa wakati wa Shughuli za Uteuzi na Uchaguzi**

33. Maadili na nidhamu ya Chama katika kusimamia na kutekeleza shughuli za uchaguzi wa Chama lazima kuzingatiwa na wale wote wanaohusika. Hivyo yawapasa kuelewa na kutambua kuwa:-

(1) Mwanachama yeyote mwenye sifa zinazohitajika, anayo haki ya kutangaza wakati wowote nia yake ya kutaka kugombea nafasi fulani. Lakini Wanachama wenye nia ya kugombea hawaruhusiwi kufanya kampeni ya aina yoyote kabla ya majina yao kuteuliwa na kikao kinachohusika.

(2) Ni mwiko kwa kiongozi mgombea au mwana CCM yeyote kutoa au kupokea rushwa. Kwa ajili hiyo, kiongozi, mgombea yeyote wakati wa uchaguzi akithibitika kuwa ametumia rushwa katika jitihada zake za kuwania nafasi anayoiomba hatateuliwa kugombea nafasi hiyo. Hali kadhalika, mgombea yeyote atakayethibitika kuwa ameshinda uchaguzi kwa njia ya kutoa rushwa, atanyang'anywa ushindi alioupata, na pia atazuiwa asigombee tena katika uchaguzi mwingine wowote kwa muda utakaoamuliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri

Kuu ya Taifa; au atapewa adhabu kubwa zaidi ya hiyo kama itakavyoonekana inafaa.

(3) Ni mwiko kwa kiongozi yeyote wa CCM kuweka mbele maslahi yake binafsi badala ya maslahi ya Chama chake pamoja na maslahi ya Taifa.

(4) Ni mwiko kwa kiongozi au mwanachama yeyote wa CCM kuunda vikundi visivyo rasmi ndani ya Chama, au kushiriki katika kampeni za uchaguzi za chini chini kinyume na Ratiba ya Uchaguzi na taratibu rasmi zilizowekwa.

(5) Ni mwiko kwa wapiga kura kupokea misaada ya usafiri, posho, n.k. kutoka kwa mgombea yeyote kwa ajili ya kuhudhuria mikutano ya uchaguzi.

(6). Ni marufuku kwa mgombea au kiongozi yeyote wa CCM kuingiza wanachama wapya kwa ufadhili wake wa kuwanunulia kadi au kuwalipia ada za uwanachama, kwa lengo la kutaka wampigie kura.

(7) Ni marufuku kwa Jumuiya yoyote inayoongozwa na Chama kujigeuza kuwa kundi la kumjenga au kumbomoa mgombea fulani.

(8 Ni marufuku kwa Kamanda yeyote wa Vijana wa CCM kutumia nafasi yake kama mbinu ya kujenga makundi ya vijana kwa malengo binafsi ya kisiasa.

(9) Katika ngazi zote za Tawi hadi Mkoa, pale ambapo kuna nafasi moja tu ya uongozi, k.m. nafasi ya Mwenyekiti au Katibu wa Halmashauri Kuu ya ngazi inayohusika; watateuliwa wagombea wasiozidi watatu, ambao watapelekwa kwenye kikao cha uchaguzi kinachohusika.

(10) Pale ambapo kuna nafasi nyingi za uongozi wa aina moja, k.m. wajumbe wa kuingia katika Halmashauri Kuu au Kamati za Siasa za ngazi zote za Tawi hadi Mkoa, watateuliwa wagombea wasiozidi mara tatu ya nafasi zinazotakiwa kujazwa.

(11) Katika ngazi ya Taifa, uteuzi wa mwisho wa wagombea nafasi za Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa orodha ya viti themanini na tano, watateuliwa wagombea wasiozidi mara tatu ya nafasi zinazotakiwa kujazwa kwa kila kundi.

(12) Ni mwiko kabisa kwa mwanachama na kwa mwombaji yeyote wa nafasi ya uongozi, kwa maneno au kwa vitendo kutumia ukabila, au dini au fedha au makaribisho ya vyakula na vinywaji au kubagua Tanzania Bara au Zanzibar katika shughuli yoyote ya Uteuzi/Uchaguzi, au kutumia jambo lolote jingine linaloweza kuvuruga Umoja na Mshikamano wa Chama au Taifa, kama njia ya kutafuta ushindi katika uchaguzi.

(13) Ni mwiko kabisa kwa kiongozi yeyote au mwombaji yeyote wa nafasi ya uongozi au mwanachama yeyote aliyekabidhiwa dhamana ya usimamizi/uangalizi wa uteuzi /uchaguzi, kufanya vitendo vya ukiukaji wa Kanuni na taratibu za uchaguzi.

(14) Ni mwiko kutumia makaratasi ya kampeni nje ya utaratibu wa Chama au kutumia vishawishi vya aina yoyote ile kwa minajili ya kupata kura.

(15) Ni mwiko kabisa kwa mgombea yeyote kufanya kampeni dhidi ya mgombea mwingine.

(16) Chama hakitaruhusu, na kwa kweli kinalaani kampeni zenye nia ya kupakana matope.

(17) Kumbukumbu za uchujaji na uteuzi wa wagombea ni siri ya Chama.

34. Kiongozi au mwanachama yeyote atakayethibitika kuwa amevunja kifungu chochote cha miiko hii atadhibitiwa. Ikibidi atanyang'anywa ushindi alioupata na kukatazwa kugombea uongozi kwa muda utakaowekwa.

# FUNGU LA PILI

## UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI YA SHINA

### Tafsiri

35. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi na Katiba ya Chama tafsiri ya maneno yaliyoorodheshwa hapa chini itakuwa kama ilivyoainishwa kwa kila neno.

"Shina" katika eneo la mitaani, maana yake ni nyumba kumi zilizohesabiwa na kuwekwa pamoja kwa madhumuni ya kuunda Shina. Isipokuwa kwamba endapo itaonekana inafaa, idadi ya nyumba inaweza kuwa zaidi kidogo ya kumi au pungufu kidogo ya hapo, ili kupata muundo mzuri kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Shina.

"Nyumba Kumi" maana yake ni Wana-CCM wasiopungua watano wanaoishi katika mazingira yafuatayo:-

(a) Katika majengo ya ghorofa ambako watu wanaishi katika Fleti, kila fleti itahesabiwa kuwa ni nyumba.

(b) Katika nyumba zilizo katika jengo moja lenye vitengo mbalimbali vya kuishi watu, kila kitengo kilichokusudiwa kuishi familia moja kitahesabiwa kuwa ni nyumba moja.

(c) Katika nyumba ya kupangisha ambako watu wanaishi katika utaratibu wa kupanga chumba

kimoja kimoja, au vyumba zaidi ya kimoja, pamoja na vyumba vya mpangaji mmoja, vitahesabiwa kuwa ni nyumba moja.

(d) Katika nyumba ambazo ziko kwenye kiwanja kimoja kimoja kwa utaratibu wa nyumba ya mwenye nyumba na nyumba ya mtumishi, zote zitahesabiwa kuwa ni nyumba mbili za wanachama tofauti. Vile vile katika maeneo yenye kaya kitakachohesabiwa ni nyumba siyo kaya. Lengo ni kutoa hadhi na heshima sawa kwa kila mwanachama wa CCM.

36. Mashina maalum ya Wakereketwa (Tanzania Bara) na Maskani (Tanzania Zanzibar) yataundwa kwa mujibu wa Ibara 22 ya Katiba ya CCM.

**Utaratibu wa Kuomba Nafasi ya Uongozi**

37. Kila mwanachama anayeishi au kufanya kazi katika Shina ambaye ametimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya Chama na ambaye anajua kusoma na kuandika kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo:-

a) Balozi/Mwenyekiti wa Shina

b) Shina lenye wanachama wasiopungua 10, litachagua wajumbe wanne wa kamati ya uongozi

38. Mwombaji nafasi ya uongozi wa Shina atajaza fomu moja iliyoandaliwa rasmi na Makao Makuu ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi na kuiwasilisha kwa Katibu wa Tawi ambamo Shina hilo limo katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi unaohusika.

39. Kamati ya Siasa ya Tawi itafikiria na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu ya Tawi juu ya wanachama wanaoomba nafasi za uongozi wa Shina katika Tawi hilo. Aidha Kamati ya Siasa ya Tawi itafikiria na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi juu ya wanachama wanaoomba nafasi za uongozi wa CCM kupitia Tawi hilo.

40. Halmashauri Kuu ya Tawi itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama walioomba kusimama katika uchaguzi huo kwa kila Shina.

41. Majina yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho yatarudishwa kwenye Shina linalohusika ili uchaguzi ufanyike kwa kuzingatia ratiba ya uchaguzi iliyopangwa.

42. Mkutano wa Mwaka wa Shina utafanyika kwa madhumuni ya uchaguzi. Utasimamiwa na Viongozi watatu walioteuliwa mapema na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi,na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

    (a) Mkutano kwanza utamchagua Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo kutoka miongoni mwa wanachama waliohudhuria. Uchaguzi huo

unaweza kufanyika kwa kunyoosha mikono na kuihesabu.

(b) Kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo kwenye mkutano huo, na wajumbe watapewa nafasi ya kumuuliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo.

43. Endapo wagombea waliopitishwa ni zaidi ya mmoja wajumbe watapiga kura za siri kumchagua kiongozi wa Shina wanayemtaka kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa madhumuni hayo.

44. Endapo kuna mgombea mmoja tu aliyepitishwa katika uteuzi wa mwisho, wajumbe wa mkutano watampigia kura za siri za “Ndiyo” au “Hapana” kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa madhumuni hayo

45. Kwa Mashina ambayo kwa mujibu wa Kanuni hizi yanatakiwa kuunda Kamati za uongozi, wanachama watamchagua kwanza kiongozi wa Shina hilo, na baada ya hapo watawachagua wajumbe wanne wa Kamati ya uongozi ya Shina.

46. Karatasi za kura kwa ajili ya uchaguzi wa wajumbe hao wanne wa Kamati ya Uongozi ya Shina zitakuwa na orodha moja tu yenye majina yasiyozidi 12 ya wagombea wote waliopitishwa katika uteuzi wa mwisho. Kwa kutumia karatasi hiyo, mpiga kura atawapigia kura za siri wajumbe wanne anaowataka.

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 40

Washindi ni wale ambao wameongoza kwa wingi wa kura tangu mshindi wa kwanza hadi wa nne maana huu ni uchaguzi wa kundi. Iwapo washindi wa nafasi ya nne ni wengi na wamelingana idadi ya kura, hao watapigiwa kura tena mpaka apatikane mwenye kura nyingi zaidi na huyo ndiye atakayekuwa mshindi wa nne.

# FUNGU LA TATU

## UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI YA TAWI

### Utaratibu wa kuomba nafasi ya Uongozi

47. Kila mwanachama anayeishi au kufanya kazi katika Tawi, ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM vifungu vya 8, 16,17 na 18 na ambaye anajua kusoma na kuandika vizuri Kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi katika Tawi:-

    (a) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi;

    (b) Katibu wa CCM wa Tawi

    (c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi

    (d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi

    (e) Wajumbe kumi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

    (f) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi;

    (g) Mjumbe mmoja mmoja wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo (Zanzibar) na Wilaya;

48. Kwa uchaguzi wa viongozi wa Tawi la mahali pa kazi ambapo wanachama wanaofanya kazi mahali hapo

hawaishi katika eneo hilo. Nafasi za uongozi wa Tawi zitaombwa na wanachama wale tu ambao ni wafanyakazi wa mahali hapo wenye ajira inayoendelea.

49. Mwombaji nafasi ya Mwenyekiti wa Tawi atajaza fomu inayohusika nakala mbili na kuiwasilisha kwa Katibu wa Tawi lenye nafasi anayoiomba, katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa ngazi ya Tawi. Aidha anayeomba nafasi nyingine za Tawi atajaza nakala mbili za fomu. Nakala moja ya fomu ya kila mwombaji itabaki kwenye kikao cha awali na ya pili kwenye kikao cha uteuzi wa mwisho.

50. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi itachunguza sifa za kila mwombaji wa nafasi zote za uongozi wa Tawi na kupeleka maoni yake juu ya waombaji wote kwenye Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi. Maoni haya yatakuwa yameandikwa kwenye fomu ya mwombaji.

51. Katika kutekeleza kazi hiyo Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi itahakikisha kwamba kila mwombaji anapewa nafasi ya kutoa maelezo yake kwenye Mkutano wa Kamati hiyo ulioitishwa kwa madhumuni hayo na kwamba inatolewa nafasi kwa wajumbe wa Kamati ya Siasa kumuuliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa, lakini hakuna mkutano mwingine wowote utakaoitishwa kumsikiliza.

52. Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba nafasi za ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo na Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya. Aidha Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi itafikiria na kutoa mapendekezo yake juu ya wanachama ambao uteuzi wao wa mwisho hufanywa na vikao vya juu kwa mujibu wa Katiba.

53. Majina yote yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho yatarudishwa kwenye Tawi linalohusika ili uchaguzi ufanyike. Katibu wa Tawi lazima awe na idadi sahihi kabisa ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Tawi.

54. Mkutano Mkuu wa Tawi utakaofanyika kwa madhumuni ya uchanguzi utasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

    (a) Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Tawi yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

    (b) Katibu wa CCM Tawi atathibitisha kutimia kwa akidi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi kwa kuwatangazia wajumbe kuwa akidi ya wajumbe wa Mkutano imetimia. Wajumbe wote wa Mkutano huo waliohudhuria wataorodheshwa majina yao. (Rejea Ibara ya 17 ya Kanuni hizi).

(c) Mara baada ya akidi ya wajumbe wa Mkutano kutimia,mkutano utamchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo. Atakayechaguliwa asiwe mmoja wa wanaogombea nafasi yoyote ya uongozi. Uchaguzi huo unaweza kufanyika kwa njia ya kunyoosha mikono juu na kuihesabu.

(d) Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Tawi watajieleza kwanza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo kwenye mkutano huo na wajumbe watapewa nafasi ya kuuliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

55. Baada ya wagombea wote kutoa maelezo yao mkutano kwanza utamchagua Mwenyekiti wa Tawi. Endapo kuna mgombea mmoja tu aliyepitishwa katika uteuzi wa mwisho, mkutano utampigia kura za siri za“Ndiyo” au “Hapana” kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa ajili hiyo. Matokeo yatahifadhiwa.

56. Mkutano utaendelea kwa utaratibu huo huo kwa uchaguzi wa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi - nafasi kumi (10) kuzingatia mgawanyo na utaratibu ufuatao:-

(i) Wagombea - kundi la wanawake - nafasi nne (4)

(ii) Wagombea - kundi la Vijana - nafasi nne (4)

(iii) Wagombea - kundi la Wazazi - nafasi mbili (2)

57. Kisha mkutano utaendelea na uchaguzi wa wajumbe wa nafasi za ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi na kisha ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo na Wilaya.

58. Uchaguzi wa wajumbe wa nafasi zote utakapomalizika na kura zao kuhesabiwa, ndipo matokeo yote kwa pamoja yatatangazwa. Matokeo ya Mwenyekiti wa Tawi yatakuwa ya mwisho kutangazwa. Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya atatangazwa kwanza.

**Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi.**

59. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Tawi utafanywa na Halmashauri Kuu ya Tawi kuwachagua wafuatao:-

(a) Katibu wa CCM wa Tawi;

(b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi

(c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi

(d) Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Tawi

Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi yatapangwa kwa kufata alfabeti. Baada ya

wagombea kujieleza, mkutano utawachagua kwanza Katibu wa Tawi, Katibu wa Siasa na Uenezi na Katibu wa Uchumi na Fedha. Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Tawi, watapatikana kutokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi ambao wataomba kwa maandishi nafasi za ujumbe huo. Isipokuwa kwamba wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi ambao moja kwa moja ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Tawi kwa mujibu wa nyadhifa zao hawataomba kugombea nafasi hii.

Endapo waombaji wa nafasi hizo watakuwa ni wengi zaidi kuliko nafasi zilizopo, Mwenyekiti na Katibu kwa pamoja wataandaa orodha ya majina yatakayopigiwa kura (kwa idadi ya mara tatu ya nafasi zilizopo). Isipokuwa kwamba katika kuifanya kazi hiyo Mwenyekiti na Katibu watazingatia umuhimu wa kupendekeza majina kutoka pande zote za Tawi; wakijielekeza kwenye maeneo yale ambayo hayakupata wajumbe wa kamati ya siasa wanaoingia moja kwa moja kutokana na nyadhifa zao.

60. Karatasi ya kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi itakuwa na orodha moja tu yenye majina yote ya wagombea na kila Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi atapiga kura ya siri kuwachagua wajumbe watano anaowataka. Ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura walizopata wagombea maana hizi ni kura za kundi. Kiwango cha kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

# FUNGU LA NNE

## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA KATA/WADI

### Utaratibu wa Kuomba Nafasi ya Uongozi

61. Mwanachama yeyote ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM vifungu vya 16, 17, na 18 ambaye anajua kusoma na kuandika vizuri Kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi katika Kata/Wadi:-

    (a) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi

    (b) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi

    (c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi

    (d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi

    (e) Wajumbe watano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi

    (f) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo

    (g) Wajumbe kumi wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya

    (h) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa mmoja kutoka kila Kata ya Tanzania Bara, na watano kutoka kila Wadi ya Tanzania Zanzibar.

62. Mwombaji nafasi ya uongozi wa Kata/Wadi atajaza fomu inayohusika na nafasi anayokusudia kuiomba na kuiwasilisha kwa Katibu wa Kata/Wadi yenye nafasi anayoiomba katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa Kata/Wadi. Anayeomba nafasi ya Mwenyekiti wa Kata/Wadi atajaza nakala mbili za Fomu.
Nakala moja ya fomu ya kila mwombaji itabaki kwenye kikao cha awali na ya pili kwenye kikao cha uteuzi wa mwisho. Utaratibu huu utafuatwa na waombaji wa nafasi zilizobaki.

63. Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba nafasi za Mwenyekiti na Katibu wa CCM Kata/Wadi, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Kata/Wadi, Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo, Wilaya na Mkoa.

**Utaratibu wa Uchaguzi:**

64. Majina yaliyoteuliwa kugombea yatarudishwa kwenye Kata/Wadi inayohusika ili uchaguzi ufanyike. Katibu wa Kata/ Wadi lazima awe na idadi kamili na sahihi ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi kwa mujibu wa Katiba ya CCM na ibara ya 17 ya Kanuni hizi.

65. Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi utakaofanyika kwa madhumuni ya uchaguzi utasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na Kamati ya Siasa ya

Halmashauri Kuu ya Wilaya, na utaendeshwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(a) Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Kata/Wadi yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

(b) Katibu wa CCM Kata/Wadi atathibitisha kutimia kwa akidi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi na kuwatangazia wajumbe kuwa akidi ya wajumbe wa Mkutano imetimia. Wajumbe wote wa Mkutano huo waliohudhuria wataorodheshwa majina yao.

(c) Mara baada ya akidi kutimia, mkutano utamchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo. Uchaguzi huo unaweza kufanyika kwa njia ya kunyoosha mikono juu na kuihesabu.

(d) Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kata/Wadi watajieleza kwanza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo mbele ya mkutano huo na wajumbe watapewa nafasi ya kuwauliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

66. Kura zitapigwa kila baada ya wagombea wa nafasi inayohusika kumaliza kujieleza na kuulizwa maswali

kama yapo. Mkutano kwanza utamchagua Mwenyekiti wa Kata/Wadi na kufuatiwa na nafasi zilizotajwa katika Ibara ya 61 ya Kanuni hizi. Endapo kuna mgombea mmoja tu wa nafasi yoyote aliyepitishwa katika uteuzi wa mwisho, mkutano utampigia kura za siri za “Ndiyo” au “Hapana” kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa ajili hiyo. Matokeo yatahifadhiwa.

67. Uchaguzi wa viongozi wa nafasi zote utakapomalizika na kura za kila nafasi kuhesabiwa, ndipo matokeo yote kwa pamoja yatatangazwa. Matokeo ya Mwenyekiti wa Kata/Wadi yatakuwa ya mwisho kutangazwa. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa watatangazwa kwanza.

**Uchaguzi wa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi.**

68. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi utafanywa na Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi kuwachagua wafuatao:-

    (a) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi

    (b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi

    (c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi

    (d) Wajumbe wa watano wa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi

Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi yatapangwa kwa kufata alfabeti. Baada ya wagombea kujieleza, mkutano utawachagua kwanza Katibu wa CCM wa Kata/Wadi, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi na Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi. Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi, watapatikana kutokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi ambao wataomba kwa maandishi nafasi za ujumbe huo. Isipokuwa kwamba wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi ambao moja kwa moja ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi kwa mujibu wa nyadhifa zao hawataomba kugombea nafasi hii.

Endapo waombaji wa nafasi hizo watakuwa ni wengi zaidi kuliko nafasi zilizopo, Mwenyekiti na Katibu kwa pamoja wataandaa orodha ya majina yatakayopigiwa kura (kwa idadi ya mara tatu ya nafasi zilizopo). Isipokuwa kwamba katika kuifanya kazi hiyo Mwenyekiti na Katibu watazingatia umuhimu wa kupendekeza majina kutoka pande zote za Kata/Wadi wakijielekeza kwenye maeneo yale ambayo hayakupata wajumbe wa kamati ya siasa wanaoingia moja kwa moja kutokana na nyadhifa zao.

69. Karatasi ya kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi itakuwa na orodha moja tu yenye majina yote ya wagombea na kila Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi atapiga kura ya siri kuwachagua wajumbe watano anaowataka. Ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 52

wa kura walizopata wagombea maana hizi ni kura za kundi. Kiwango cha Kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 53

# FUNGU LA TANO

## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA JIMBO (ZANZIBAR)

### Utaratibu wa Kuomba Nafasi ya Uongozi

70. Mwanachama yeyote ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM vifungu vya 16, 17, na 18 ambaye anajua kusoma na kuandika vizuri Kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi wa Jimbo:-

    (a) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo

    (b) Katibu wa CCM wa Jimbo

    (c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo

    (d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo

    (e) Wajumbe watano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

    (f) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya

    (g) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa kutoka kila Wadi ya Jimbo linalohusika.

71. Mwombaji wa nafasi ya uongozi wa Jimbo atajaza fomu inayohusika na nafasi anayokusudia kuiomba

na kuiwasilisha kwa Katibu wa Jimbo lenye nafasi anayoiomba katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa Jimbo.

Anayeomba nafasi ya Mwenyekiti wa Jimbo atajaza nakala mbili za Fomu. Nakala moja ya fomu ya kila mwombaji itabaki kwenye kikao cha awali na ya pili kwenye kikao cha uteuzi wa mwisho. Utaratibu huu utafuatwa na waombaji wa nafasi zilizobaki.

72. Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wana Chama wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo Katibu wa Itikadi na Uenezi, Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo,Wilaya na Mkoa.

**Utaratibu wa Uchaguzi:**

73. Majina yaliyoteuliwa kugombea yatarudishwa kwenye Jimbo linalohusika ili uchaguzi ufanyike. Katibu wa Jimbo lazima awe na idadi kamili na sahihi ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa mujibu wa Katiba ya CCM na ibara ya 17 ya Kanuni hizi.

74. Mkutano Mkuu wa Jimbo utakaofanyika kwa madhumuni ya uchaguzi utasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya, na utaendeshwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(a) Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Jimbo yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

(b) Katibu CCM wa Jimbo atathibitisha kutimia kwa akidi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo na kuwatangazia wajumbe kuwa akidi ya wajumbe wa Mkutano imetimia. Wajumbe wote wa Mkutano huo waliohudhuria wataorodheshwa majina yao.

(c) Mara baada ya akidi kutimia, mkutano utamchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo. Uchaguzi huo unaweza kufanyika kwa njia ya kunyoosha mikono juu na kuihesabu.

(d) Wajumbe wa nafasi ya Mwenyekiti wa Jimbo watajieleza kwanza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo mbele ya mkutano huo na wajumbe watapewa nafasi ya kumuuliza maswali yasiyozidi matatu kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

75. Kura zitapigwa kila baada ya wagombea wa nafasi inayohusika kumaliza kujieleza na kuulizwa maswali kama yapo. Mkutano kwanza utamchagua Mwenyekiti wa Jimbo na kufuatiwa na nafasi zilizotajwa katika Ibara ya 70 ya Kanuni hizi. Endapo kuna mgombea mmoja tu wa nafasi yoyote aliyepitishwa katika uteuzi wa mwisho, mkutano

utampigia kura za siri za “Ndiyo” au “Hapana” kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa ajili hiyo. Matokeo yatahifadhiwa.

76. Uchaguzi wa viongozi wa nafasi zote utakapomalizika na kura za kila nafasi kuhesabiwa, ndipo matokeo yote kwa pamoja yatatangazwa. Matokeo ya Mwenyekiti wa Jimbo yatakuwa ya mwisho kutangazwa. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa watatangazwa kwanza.

**Uchaguzi wa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Jimbo**

77. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Jimbo utafanywa na Halmashauri Kuu ya Jimbo kuwachagua wafuatao:-

    (a) Katibu wa CCM wa Jimbo

    (b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo

    (c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo

    (d) Wajumbe wa watano wa Kamati ya Siasa ya Jimbo

    Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi yatapangwa kwa kufata alfabeti. Baada ya wagombea kujieleza, mkutano utawachagua kwanza Katibu wa CCM wa Jimbo, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo na Katibu wa Uchumi na Fedha wa

Jimbo. Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Jimbo, watapatikana kutokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Jimbo ambao wataomba kwa maandishi nafasi za ujumbe huo. Isipokuwa kwamba wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Jimbo ambao moja kwa moja ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Jimbo kwa mujibu wa nyadhifa zao hawataomba kugombea nafasi hii.

Endapo waombaji wa nafasi hizo watakuwa ni wengi zaidi kuliko nafasi zilizopo, Mwenyekiti na Katibu kwa pamoja wataandaa orodha ya majina yatakayopigiwa kura (kwa idadi ya mara tatu ya nafasi zilizopo). Isipokuwa kwamba katika kuifanya kazi hiyo Mwenyekiti na Katibu watazingatia umuhimu wa kupendekeza majina kutoka pande zote za Jimbowakijielekeza kwenye maeneo yale ambayo hayakupata wajumbe wa kamati ya siasa wanaoingia moja kwa moja kutokana na nyadhifa zao.

78. Karatasi ya kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Jimbo itakuwa na orodha moja tu yenye majina yote ya wagombea na kila Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Jimbo atapiga kura ya siri kuwachagua wajumbe watano anaowataka. Ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura walizopata wagombea maana hizi ni kura za kundi. Kiwango cha Kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi, ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

# FUNGU LA SITA

## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA WILAYA

### Utaratibu wa Kuomba Nafasi ya Uongozi

79. Mwanachama yeyote ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM vifungu vya 8, 16,17 na 18 na ambaye anajua kusoma na kuandika vizuri Kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi wa Wilaya:-

    (a) Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya

    (b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya

    (c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya

    (d) Wajumbe kumi wa Halmashauri Kuu ya Wilaya

    (e) Wajumbe wawili wa Mkutano Mkuu wa Mkoa

    (f) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa

80. (a) Mwombaji wa nafasi ya uongozi wa ngazi ya Wilaya atajaza fomu inayohusika kwa nafasi anayoiomba, na kuwasilisha fomu yake kwa Katibu wa CCM wa Wilaya yenye nafasi anayoiomba katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa ngazi ya Wilaya. Waombaji wa nafasi ya Mwenyekiti wa Wilaya watajaza nakala mbili za fomu kila mmoja. Waombaji wa nafasi zilizobaki watajaza

nakala mbili pia za fomu kila mmoja. Nakala moja ya fomu itabaki kwenye kikao cha awali kinachowajadili waombaji na ya pili itahifadhiwa na kikao cha uteuzi wa mwisho.

(b) Kwa uchaguzi unaohusu Wilaya za CCM za Vyuo vya Elimu ya Juu, ni mwanachama anayesoma katika Chuo cha Elimu ya Juu ndiye atakayekuwa na haki ya kuomba nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa aliyechaguliwa kutoka wilaya ya Vyuo vya Elimu ya Juu.

81. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi na Katiba ya Chama, Wilaya ya CCM ya Vyuo vya Elimu ya Juu itakuwa na maana ifuatayo:

(a) Wilaya za Vyuo vya Elimu ya Juu zitaundwa na Matawi ya Vyuo Vikuu vilivyomo katika Kanda ambazo zimeorodheshwa hapa chini.

i. Kanda ya Dar es Salaam
ii. Kanda ya Mashariki ambayo itakuwa na mikoa ya Pwani, Morogoro na Tanga
iii. Kanda ya Kusini ambayo itakuwa na mikoa ya Lindi na Mtwara
iv. Kanda ya Nyanda za juu Kusini, mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa
v. Kanda ya Kati, mikoa ya Dodoma na Singida
vi. Kanda ya Kaskazini, mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara
vii. Kanda ya Ziwa, mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga

viii. Kanda ya Magharibi, mikoa ya Kigoma na Tabora

(b) Kwa kuzingatia kwamba muda wa kuwa mwanafunzi katika Wilaya na Mkoa wa Vyuo vya Elimu ya Juu ni Maalum, Kamati Kuu itatoa mwongozo kwa wakati husika utakaotumika katika kufanya uteuzi wa mwisho wa wana CCM watakaoomba nafasi ya uongozi katika ngazi ya Wilaya na Mkoa wa Vyuo vya Elimu ya Juu.

82. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya itachunguza sifa za waombaji wa nafasi zote za uongozi wa ngazi hii ya Wilaya. Katika kuitekeleza kazi hiyo, Kamati ya Siasa itahakikisha kwamba kila mwombaji anapewa nafasi ya kutoa maelezo yake na kwamba inatolewa nafasi kwa wajumbe wa Kamati ya Siasa kumuuliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

83. Baada ya uchunguzi kuhusu sifa za waombaji kukamilika, Kamati ya Siasa Wilaya itatoa mapendekezo yake juu ya kila mwombaji kwenye fomu sehemu inayohusika. Mapendekezo ya kikao yatafikishwa kwenye kikao cha Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa.

84. Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho kwa waombaji wa nafasi zifuatazo:-

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Wilaya, Katibu wa Uchumi na Fedha wa CCM Wilaya, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM wa Wilaya na Mkoa, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kupitia Wilaya hiyo.

85. Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya za Tanzania Zanzibar.

86. Kamati Kuu itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa uteuzi wa mwisho juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

**Utaratibu wa Uchaguzi**

87. Majina yote yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho na vikao vinavyohusika yatarejeshwa kwenye Wilaya inayohusika ili uchaguzi ufanyike. Katibu wa CCM wa Wilaya lazima awe na idadi sahihi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya wanaopaswa kuhudhuria mkutano huo.

88. Mkutano Mkuu wa Wilaya utakaofanyika kwa madhumuni ya uchaguzi utasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na Kamati ya Siasa ya Mkoa na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

    (a) Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Wilaya yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

(b) Katibu wa CCM wa Wilaya atathibitisha kutimia kwa akidi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya. Atafanya hivyo kwa kuwatangazia wajumbe kwamba akidi ya wajumbe wa Mkutano imetimia (ibara ya 17 ya Kanuni hizi inahusika).

(c ) Kazi ya kwanza baada ya akidi ya wajumbe kutimia, itakuwa kumchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa muda unaweza kufanyika kwa njia ya kuinua mikono na kuihesabu.

(d) Waombaji wa nafasi ya Mwenyekiti wa Wilaya watajieleza kwanza, kila mmoja atapewa nafasi ya kujieleza mbele ya Mkutano,na wajumbe watapewa nafasi ya kumuuliza maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Kisha kura zitapigwa na matokeo ya uchaguzi yatahifadhiwa. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza

(e) Mkutano utaendelea kwa utaratibu huo huo kwa uchaguzi wa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya nafasi kumi kwa kuzingatia mgawanyo na utaratibu ufuatao:-

(i) Wagombea - kundi la WANAWAKE - nafasi nne (4)

(ii) Wagombea - kundi la VIJANA - nafasi nne (4)

(iii) Wagombea - kundi la WAZAZI - nafasi mbili (2)

(f) Kisha Mkutano utaendelea na utaratibu huo huo kwa uchaguzi wa wajumbe wawili (2) wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, na wajumbe watano (5) wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM Taifa.

(g) Uchaguzi wa Wajumbe wa nafasi zote ukimalizika na kura zote kuhesabiwa ndipo matokeo ya kura kwa nafasi zote yatatangazwa kwa pamoja. Matokeo ya nafasi ya Mwenyekiti wa Wilaya yatatangazwa mwisho.

**Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya**

89. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Wilaya utafanywa na Halmashauri Kuu ya Wilaya kuwachagua wafuatao:-

(a) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya

(b) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya

(c) Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Wilaya

Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi yatapangwa kwa kufata alfabeti. Baada ya wagombea kujieleza, mkutano utawachagua kwanza Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya na Katibu wa

Uchumi na Fedha wa Wilaya. Wajumbe watano wa Kamati ya Siasa ya Wilaya, watapatikana kutokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ambao wataomba kwa maandishi nafasi za ujumbe huo. Isipokuwa kwamba wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ambao moja kwa moja ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya kwa mujibu wa nyadhifa zao hawataomba kugombea nafasi hii.

Endapo waombaji wa nafasi hizo watakuwa ni wengi zaidi kuliko nafasi zilizopo, Mwenyekiti na Katibu kwa pamoja wataandaa orodha ya majina yatakayopigiwa kura (kwa idadi ya mara tatu ya nafasi zilizopo). Isipokuwa kwamba katika kuifanya kazi hiyo Mwenyekiti na Katibu watazingatia umuhimu wa kupendekeza majina kutoka pande zote za Wilaya: wakijielekeza kwenye maeneo yale ambayo hayakupata wajumbe wa kamati ya siasa wanaoingia moja kwa moja kutokana na nyadhifa zao.

90. Karatasi ya kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya itakuwa na orodha moja tu yenye majina yote ya wagombea na kila Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya atapiga kura ya siri kuwachagua wajumbe watano anaowataka kwa kila wilaya ya Bara na watatu kwa kila wilaya ya Zanzibar. Ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura walizopata wagombea maana hizi ni kura za kundi. Kiwango cha Kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi, ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 65

# FUNGU LA SABA

## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA MKOA

### Utaratibu wa Kuomba Nafasi ya Uongozi

91. Mwanachama yeyote ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM vifungu vya 8, 16, 17 na 18 na ambaye anajua kusoma na kuandika vizuri Kirumi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi wa Mkoa:-

    (a) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa

    (b) Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, nafasi ya Mkoa
        i. Mjumbe mmoja kwa Mkoa wa Bara

        ii. Wajumbe wanne kwa Mkoa wa Tanzania Zanzibar

    (c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Mkoa

    (d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Mkoa

    (e) Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa:-

        i. Wajumbe wawili kutoka kila Wilaya za Mkoa wa Bara,

        ii. Wajumbe watano kutoka kila Wilaya za Mkoa wa Zanzibar

92. Waombaji wa nafasi hizo watajaza fomu inayohusika. Waombaji wa nafasi za Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa watawasilisha fomu zao kwa Katibu wa Chama wa Wilaya wanakoishi au kufanya kazi. Waombaji wa nafasi ya Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa watawasilisha fomu zao kwa Katibu wa Chama wa Mkoa wanakoomba nafasi hiyo. Waombaji wa nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa Ngazi ya Mkoa watawasilisha Fomu zao kwa Katibu wa Chama wa Mkoa anakoomba nafasi hiyo. Fomu hizo zitawasilishwa katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi unaohusika. Waombaji wote wa nafasi hizi watajaza nakala mbili za fomu kila mmoja. Nakala moja ya fomu ya mwombaji itabaki kwenye kikao cha awali kinachowajadili waombaji wa nafasi hizi baada ya kuandika maoni ya vikao vinavyowafikiria. Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (Zanzibar) itabaki na nakala moja ya fomu ya kila mwombaji nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa. Nakala ya tatu itahifadhiwa na kikao cha uteuzi wa mwisho wa wagombea.

**Utaratibu wa Kuchuja Majina ya Waombaji**

93. Waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa wataanza kujadiliwa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya wanakoishi au kufanya kazi. Kamati ya Siasa ya Wilaya itatoa maoni na mapendekezo yake juu ya waombaji kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa.

94. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa itachunguza sifa za waombaji wa Nafasi ya Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mkoa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa; na kutoa mapendekezo ya kila muombaji kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa upande wa Zanzibar, mapendekezo ya Kamati ya Siasa ya Mkoa juu ya waombaji wa nafasi ya Katibu wa Uchumi na Fedha wa MKoa, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mkoa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa, yatawasilishwa kwenye kikao cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ambayo itawajadili na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu.

95. Kamati Kuu itajadili kwa pamoja waombaji wa nafasi zote za wagombea wa Mikoa ya Tanzania Bara na Mikoa ya Tanzania Zanzibar na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

96. Halmashauri Kuu ya Taifa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa waombaji wa nafasi hizi.

**Utaratibu wa Uchaguzi**

97. Majina yote yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho wa vikao vinavyohusika yatafikishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa ili uchaguzi ufanyike. Mkutano Mkuu wa Mkoa utafanyika kwa madhumuni ya uchaguzi na utasimamiwa na viongozi wawili au

watatu walioteuliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Mkoa yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

(b) Katibu wa Mkoa atathibitisha kwamba akidi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa imetimia. Katibu wa Mkoa atafanya hivyo kwa kuwatangazia Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kwamba akidi ya wajumbe wa Mkutano imetimia kwa mujibu wa Katiba ya Chama na ibara ya 17 ya Kanuni hizi inahusika.

(c) Kazi ya kwanza baada ya akidi ya mkutano kutimia itakuwa ni kumchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa muda unaweza kufanyika kwa njia ya kunyoosha mikono juu na kuihesabu.

(d) Baada ya hapo mkutano utaanza kuwasikiliza mgombea mmoja mmoja wakijieleza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kuulizwa maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

(e) Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa watajieleza kwanza na mara baada ya maelezo

yao wote, kura zitapigwa. Kisha mkutano utaendelea na utaratibu huo huo kwa nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ngazi ya Mkoa na Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa.

(f) Matokeo ya kura yatatangazwa yote kwa pamoja baada ya kura za waombaji wa nafasi zote kuhesabiwa. Matangazo ya matokeo yataanza na nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa kutoka ngazi ya Wilaya, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na kumalizia na matokeo ya Mwenyekiti wa Mkoa.

**Uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa**

98. Uchaguzi wa Kamati ya Siasa ya Mkoa utafanywa na Halmashauri Kuu ya Mkoa kuwachagua wafuatao:-

(a) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa

(b) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa

(c) Wajumbe wa watano wa Kamati ya Siasa ya Mkoa

Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi yatapangwa kwa kufuata alfabeti. Baada ya wagombea kujieleza, mkutano utawachagua kwanza Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa na Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa. Wajumbe watano wa

Kamati ya Siasa ya Mkoa, watapatikana kutokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa ambao wataomba kwa maandishi nafasi za ujumbe huo. Isipokuwa kwamba wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa ambao moja kwa moja ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa kwa mujibu wa nyadhifa zao hawataomba kugombea nafasi hii.

Endapo waombaji wa nafasi hizo watakuwa ni wengi zaidi kuliko nafasi zilizopo, Mwenyekiti na Katibu kwa pamoja wataandaa orodha ya majina yatakayopigiwa kura (kwa idadi ya mara tatu ya nafasi zilizopo). Isipokuwa kwamba katika kuifanya kazi hiyo Mwenyekiti na Katibu watazingatia umuhimu wa kupendekeza majina kutoka pande zote za Mkoa wakijielekeza kwenye maeneo yale ambayo hayakupata wajumbe wa kamati ya siasa wanaoingia moja kwa moja kutokana na nyadhifa zao.

99. Karatasi ya kura kwa ajili ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa itakuwa na orodha moja tu yenye majina yote ya wagombea na kila Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa atapiga kura ya siri kuwachagua wajumbe watano anaowataka kwa kila Mkoa wa Tanzania Bara na watatu kwa kila Mkoa wa Tanzania Zanzibar. Ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura walizopata wagombea maana hizi ni kura za kundi. Kiwango cha Kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi, ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 71

# FUNGU LA NANE

## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA TAIFA

### Utaratibu wa kuomba nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa

100. Mwanachama yeyote ambaye anatimiza masharti yote ya uanachama pamoja na sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya Chama, vifungu vya 8, 16, 17 na 18 na ambaye anajua kusoma na kuandika Kirumi barabara anayo haki ya kuomba nafasi ya uongozi ya ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

101. Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa unaohusika kwa maana ya kifungu hiki ni wa aina mbili zifuatazo:-

(a) Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, nafasi themanini na tano orodha ya Taifa;

(b) Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, orodha ya Mikoa

102. Mwombaji atajaza “Fomu” maalum zilizoandaliwa kwa ajili hiyo na kuziwasilisha kwa Katibu wa Mkoa anakoishi au kufanya kazi. Ataiwasilisha fomu yake katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa ngazi hii ya Taifa.

**Utaratibu wa kuwachuja waombaji wa nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa:**

103. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa itachunguza sifa za waombaji wa nafasi hii ya ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na kupeleka maoni na mapendekezo yake kwa Kamati Kuu. Kwa upande wa Zanzibar, mapendekezo ya Kamati ya Siasa ya Mkoa juu ya waombaji wa nafasi hizi yatawasilishwa kwenye kikao cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ambayo itawafikiria na kutoa mapendekezo yake kwenye Kamati Kuu.

104. Kamati Kuu itachunguza sifa za waombaji wa nafasi za ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa pamoja kutoka Bara na Zanzibar na kuwasilisha mapendekezo yake juu ya waombaji wote kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa.

105. Halmashauri Kuu ya Taifa itawafikiria waombaji hawa na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa nafasi hizi.

**Utaratibu wa kupendekeza Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM**

106. Kwa nafasi za Mwenyekiti wa CCM, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara na Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Zanzibar; Kamati Kuu itafikiria na kupendekeza majina ya wana-CCM watakaosimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa

Chama na majina ya wana-CCM watakaosimama katika Uchaguzi wa Makamu wawili wa Mwenyekiti wa Chama na kuwasilisha mapendekezo yake kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa. Wanaopendekezwa hawajazi fomu za kuomba kugombea nafasi hizi (Rejea ibara namba moja ya Kanuni hizi).

107. Halmashauri Kuu ya Taifa itapokea majina ya wana-CCM waliopendekezwa na Kamati Kuu kugombea nafasi za uongozi zilizotajwa hapo juu na kufanya uteuzi wa mwisho wa jina moja kwa kila nafasi. Walioteuliwa watapigiwa kura na Mkutano Mkuu wa Taifa ili kuwachagua.

**Utaratibu wa Uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa pamoja na Mwenyekiti wa CCM na Makamu wake wawili.**

108. Majina yote ya wagombea wa ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa orodha ya viti themanini na tano (85) yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho na Halmashauri Kuu ya Taifa yatafikishwa kwenye Mkutano Mkuu ili uchaguzi ufanyike. Majina yote ya wagombea Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa orodha ya Mikoa yaliyoteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa yatarudishwa Mikoani ili uchaguzi ufanywe na Mkutano Mkuu wa kila Mkoa.

109. Mkutano Mkuu wa Taifa wa uchaguzi utasimamiwa na Kamati Maalum ya Uchaguzi itakayopendekezwa na Halmashauri Kuu ya Taifa siku ya uteuzi wa majina

ya wagombea na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa siku ya kikao cha uchaguzi. Mkutano huu wa uchaguzi utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Majina ya wagombea wa nafasi hizi za uongozi yawe yameandaliwa mapema kufuata alfabeti.

(b) Mkutano utawasikiliza wagombea wote wa ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, orodha ya viti themanini na tano 85 wakijieleza kwanza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo yake na wajumbe wa mkutano watapewa nafasi ya kumuuliza maswali yasiyozidi matatu (3), kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile mwombaji hatahudhuria mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

(c) Orodha hiyo ya Taifa ya viti themanini na tano (85) itagawanywa katika makundi matano yafuatayo, na kwa kila kundi majina ya wagombea yapangwe kufuata alfabeti:-

(i) Wagombea - kundi la WANAWAKE - nafasi ishirini (20) -(Bara 13 na Zanzibar 7)

(ii) Wagombea - kundi la VIJANA - nafasi kumi na tano (15) - (Bara 9; Zanzibar 6). Umri wao ni kuanzia miaka 18 hadi 30.

(iii) Wagombea - kundi la WAZAZI - nafasi kumi 10 (Bara 6 na Zanzibar 4)

(iv) Wagombea - kundi la Zanzibar - nafasi ishirini (20).

(v) Wagombea - kundi la Bara - nafasi ishirini (20).

(d) Uchaguzi wa wagombea wa makundi yaliyoainishwa hapo juu utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

Katika awamu ya kwanza wagombea wa kundi la Wanawake watajieleza mmoja baada ya mwingine. Wajumbe watapewa nafasi ya kumuuliza kila mgombea maswali yasiyozidi matatu (3) , kama yapo,. Baada ya maelezo yao, kura zitapigwa. Kisha Mkutano utaendelea kusikiliza maelezo ya wagombea wa kundi la Vijana na kuwapigia kura. Mkutano utaendelea kwa utaratibu huo huo kwa kundi la Wazazi, kundi la Zanzibar na mwisho kundi la Bara.

110. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ataongoza mkutano katika shughuli zote za uchaguzi isipokuwa uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu wawili wa Mwenyekiti wa Chama.

111. Baada ya uchaguzi wa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kumalizika, Mwenyekiti na Makamu wawili wa Mwenyekiti wa Chama wataondoka kwenye viti vyao na kujiunga na wajumbe wengine wa mkutano. Mkutano utamchagua Mwenyekiti wa muda kutoka miongoni mwao ili uchaguzi wa kujaza

nafasi zao ufanyike chini ya usimamizi wa Kamati Maalum ya Uchaguzi.

112. Kwanza mkutano utapiga kura za siri za “Ndiyo” au “Hapana” kwa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Chama. Kura hizo zitapigwa kwa kutumia karatasi za kura zilizoandaliwa mapema kwa ajili hiyo. Utafuata uchaguzi wa makamu wawili wa Mwenyekiti.

113. Matangazo ya matokeo ya uchaguzi wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa - orodha ya viti themanini na tano (85), Makamu wawili wa Mwenyekiti na Mwenyekiti wa CCM yatatangazwa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa - orodha ya viti themanini na tano yatatangazwa kwanza kwa utaratibu uliofuatwa wakati wa kupiga kura, kwa kuanza na matokeo ya Kundi la Wanawake.

(b) Yatafuata matangazo ya matokeo ya uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa Chama upande wa Bara. Mwisho yatatangazwa matokeo ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Chama.

**Uchaguzi wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa**

114. Uchaguzi wa wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa utafanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa kutokana na orodha ya majina yasiyozidi

thelathini (30) iliyotayarishwa na Mwenyekiti wa Chama kutoka miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ili kupata wajumbe wa nafasi 14 za Kamati Kuu. Utaratibu wa uchaguzi utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Wajumbe watapiga kura kuwachagua wajumbe saba (7) kutoka Zanzibar wakiwemo wanawake waliochaguliwa wasiopungua wawili.

(b) Kisha wajumbe watapiga kura kuwachagua wajumbe saba (7) kutoka Tanzania Bara wakiwemo wanawake waliochaguliwa wasiopungua wawili.

(c) Katika uchaguzi huu majina ya wagombea yataandikwa kwa kufuata alfabeti.

(d) Wajumbe wengine wa Kamati Kuu watapatikana kwa mujibu wa Katiba ya CCM katika vifungu vinavyohusika.

**Uchaguzi wa Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu wa Chama na Wakuu wa Idara Makao Makuu ya Chama.**

115. Kwa mujibu wa Katiba ya CCM kifungu cha 107 (13) (d) Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu wa Chama na Wakuu wa Idara Makao Makuu ya Chama watachaguliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka miongoni mwao.

Mwenyekiti wa Chama atapendekeza jina moja kwa kila nafasi kwa kuzingatia kwamba Naibu Katibu Mkuu wa CCM atakayefanyia kazi Tanzania Bara atatoka Bara. Na atakayefanyia kazi Tanzania Zanzibar atatoka Zanzibar.

116. Maelezo binafsi ya kila mgombea yatawasilishwa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa watampigia kila mmoja kura za “Ndiyo” au “Hapana”.

**Uteuzi wa Makatibu wa Chama wa Mikoa**

117. Makatibu wa CCM wa Mikoa watateuliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa mujibu wa ibara ya 107(12) ya Katiba kutoka orodha iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Chama kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

# FUNGU LA TISA

## MENGINEYO

### Uchaguzi wa Kujaza Nafasi zilizoachwa Wazi

118. Nafasi ya uongozi itakuwa imeachwa wazi endapo litatokea mojawapo katika matukio yafuatayo kumhusu kiongozi aliyekuwa ameshika nafasi hiyo:-

(a) Atajiuzulu mwenyewe

(b) Atafariki dunia

(c) Ataachishwa au atafukuzwa uongozi kwa mujibu wa Katiba ya Chama

(d) Atang atuka/kustaafu.

(e) Atajiunga na Chama kingine chochote cha Siasa.

(f) Kulihama eneo la uongozi wa ngazi yake au Tawi lake maalum na hivyo kuwa nje ya upeo wa madaraka ya kikao ambacho kabla ya kuhama alikuwa mjumbe wake. Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mkutano Mkuu wa Taifa hawafungwi na sababu hii kwa maana upeo wa uongozi wao ni nchi nzima.

119. Mara baada ya nafasi ya kiongozi kuwa wazi, Katibu wa Chama wa ngazi yenye nafasi hiyo atafanya mambo yafuatayo Kwa idhini ya Katibu wa Kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa nafasi hiyo iliyoachwa wazi:-

    (i) Atatangaza nafasi hiyo ili wanachama wanaopenda na wenye sifa bora za uongozi kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi waweze kujaza fomu za kuomba uongozi huo.

    (ii) Ataweka ratiba ya uchaguzi wa kujaza nafasi hiyo.

120. Ratiba ya Uchaguzi wa kujaza nafasi ya uongozi iliyoachwa wazi itapaswa kuzingatia yafuatayo:-

    (a) Kwanza nafasi yoyote ya uongozi inapoachwa wazi inatakiwa ijazwe kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

    (b) Kwamba maelekezo ya Kanuni za Uchaguzi wa Chama na maelekezo ya Katiba ya Chama juu ya ujazaji wa nafasi za uongozi zinapoachwa wazi katika ngazi mbalimbali za uongozi wa Chama yanatekelezwa ipasavyo.

    (c) Katibu wa Chama anayeandaa uchaguzi wa kujaza nafasi wazi iliyotokea, awasilishe haraka ratiba hiyo ya uchaguzi kwa Katibu wa Kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho wa wagombea ili tangazo la kujaza nafasi hiyo liwe ndani ya

ratiba ya uchaguzi utakaotolewa idhini ya kutangazwa.

**Kugawanywa kwa Kijiji, Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya na Mkoa**

121. Endapo Kijiji, Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya au Mkoa utagawanywa katika maeneo mawili au zaidi kwa mujibu wa Sheria na taratibu za nchi, basi Wajumbe wa Vikao vyote vya CCM ambao walichaguliwa na Mkutano Mkuu wa eneo la awali kabla ya kugawanywa wataendelea na ujumbe wao hata baada ya mgawanyo huo kutamkwa rasmi na mamlaka zinazohusika. Aidha, vikao vya Chama vinavyohusika vitaendelea kutenda kazi zake ikiwa ni pamoja na maandalizi yote ya shughuli za uchaguzi wa viongozi wa Chama wa maeneo mapya yanayotokana na mgawanyo wa eneo la awali.

122. Wajumbe hao watakuwa wamekamilisha shughuli zao siku ya Mkutano Mkuu wa ngazi inayohusika wakati uongozi mpya utakapokuwa umechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Chama. Isipokuwa kwamba pale ambapo Halmashauri Kuu ya Taifa itaamua vinginevyo, utaratibu huu utafuatwa katika ngazi zote za uongozi wa Chama ambako mgawanyo wa maeneo hayo utafanywa.

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 82

**".....Uongozi si kazi ingawa zipo kazi za uongozi. Hivyo Wajumbe wa Vikao vya Chama ni lazima wawe na kazi zao za kawaida kama ajira au kilimo ama wawe na kazi za uongozi katika Chama, Serikali au Mashirika ya Umma. Vinginevyo kutakuwa na watu katika Chama ambao si Wakulima wala si Wafanyakazi na huo ndio mwanzo wa kujenga kundi la Wababaishaji wa kisiasa ndani ya Chama, jambo ambalo ni hatari sana kwa harakati za Ujamaa".**

**(Mwongozo wa CCM 1981)**

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 83

KANUNI ZA UCHAGUZI WA CCM FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:55 PM Page 84